**Mpango wa Watoto Wachanga wa North Carolina**

# Maswali Yanayoulizwa Sana Ukaguzi wa Kifedha na Marekebisho ya Hali ya Ugumu wa Maisha

1. **Kwa nini mpango wa ITP una utaratibu wa ukaguzi wa kifedha na marekebisho ya hali ya ugumu wa maisha?**
   Utaratibu huu huhakikisha kuwa mabadiliko mahususi katika hali ya kifedha ya familia yanazingatiwa, panapohitajika, ili kutambua uwezo wa familia wa kulipia huduma. Uwezo wa kulipia huduma hutambuliwa na Kipimo cha Ada Inayobadilika ya ITP (SFS, Sliding Fee Scale). SFS hulingana na ukubwa na mapato ya jumla ya familia yaliyorekebishwa na kuthibitishwa (AGI, Adjusted Gross Income).

2. **Ni kwa hali gani mahususi za kifedha ambapo ninaweza kuomba kurekebishwa kwa hali ya ugumu wa maisha?**
   Ombi la kurekebishwa kwa hali ya ugumu wa maisha linaweza kuwasilishwa kwa mabadiliko ambayo yanaweza kuathiri zaidi uwezo wa familia wa kulipia huduma. Aina za hali ya ugumu wa maisha ni kupoteza makao, kupoteza kazi/mapato au gharama kubwa za matibabu ya kujilipia mwaka ya husika.

3. **Ninawezaje kuomba marekebisho ya hali ya ugumu wa maisha?**
   Jaza Fomu ya Maombi ya Ukaguzi wa Kifedha na Marekebisho ya Hali ya Ugumu wa Maisha ili uanzishe utaratibu huu. Mratibu wa huduma yako anaweza kukusaidia katika utaratibu huu.

4. **Ni hati gani za uthibitishaji zinazohitajika ili kutuma ombi?**
   Hapa chini kuna baadhi ya mifano ya kila aina ya hali ya ugumu wa maisha. Ofisi kuu ya CDSA inaweza kuomba maelezo zaidi ya uthibitishaji.

   Kupoteza Makao:

   - Madai ya bima ya hali ya kupoteza makao kabisa/kupoteza makao kwa kiwango kikubwa inayohitaji familia kuhama
   - Hati ya benki ya hatua inayohitaji kuchukuliwa, ikiwa nyumba imechukuliwa na benki,

   Kupoteza Ajira au Njia ya Mapato:

   - Maelezo ya kutoajiriwa na maelezo mengineyo ya manufaa
   - Taarifa kutoka kwa mwajiri
   - Ikiwa hakuna barua ya uthibitishaji ya mwajiri, familia inaweza kuwasilisha barua iliyo na:
     - jina la mwajiri wa zamani
     - maelezo ya mawasiliano
     - tarehe ya mabadiliko katika ajira
     - kiasi cha mapato yaliyopotea

     Ikiwa CDSA inaweza kuthibitisha maelezo hayo, yanaweza kutumika kurekodi mahitaji.

   Gharama Kubwa za Matibabu ya Kujilipia:

   - Gharama za matibabu lazima:
     - zitokee katika mwaka husika
     - zisilipwe kutoka kwenye Akaunti ya Akiba ya Afya
     - Jumla ya gharama za kujilipia lazima ifikie au izidi asilimia ya sasa ya AGI inayotumika na Huduma ya Mapato ya Ndani (Internal Revenue Service), pamoja na kutimiza ufafanuzi wa IRS wa gharama za matibabu zinazoruhusiwa. Kwa asilimia ya sasa ya AGI na ufafanuzi wa gharama za matibabu zinazoruhusiwa, tafadhali soma *Maagizo ya Ratiba ya A* kwenye tovuti ya IRS (irs.gov).
   - Bili za matibabu, risiti za malipo yaliyofanywa na ufafanuzi wa manufaa (EOB, Explanation of Benefits)
   - Maelezo ya mpango wa bima/kadi ya mteja ikiwa hayapo kwenye faili ya CDSA

## 5. Nitajua lini kama ombi langu limeidhinishwa?

Lazima CDSA ifanye uamuzi ndani ya siku 30 kuanzia tarehe ya kupokelewa kwa hati zote zinazohitajika za kutuma ombi. CDSA itathibitisha wakati ambapo hati zote zinazohitajika zinapokelewa. Tarehe hii itawekwa kwenye fomu ya maombi. Utapokea barua ya kukufahamisha kuhusu hali ya ombi lako. Mkutano wa IFSP utafanyika, panapohitajika, ili kupitia uamuzi uliofanywa, kusasisha mpango wa IFSP, na kujaza fomu za fedha. Familia inaweza kufuata utaratibu wa kuwasilisha malalamiko kwa jimbo iwapo kutakuwa na migogoro.